

# Kijarida cha Mountain View

## Oktoba 2, 2019

**Ijumaa, Oktoba 11.....Wazazi na /Baraza la Jumuiya ya Shule, 8:30, CLC**  
**Alhamisi, Oktoba 17.....Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani**  
**Ijumaa, Oktoba 18.....Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani**  
**Jumatatu, Oktoba 21.....Hakuna Shule, Mapumziko ya Majira ya Kupukutika kwa Majani**

### Ujumbe wa Mwalimu Mkuu

Ningependa kutumia kijarida hiki kama nafasi ya kushukuru Kampuni ya Williams, mshirika wa biashara wa muda mrefu wa Shule ya Msingi ya Mountain View. Hivi maajuzi walitoa kwa ukarimu \$10,000 kwa shule yetu ili kuunga mkono masomo na maendeleo ya wanafunzi. Wafanyakazi kadhaa wa Williams na wapenzi wao wanahudumu pia kama watu wa kujitolea katika shule ya msingi ya Mountain View. Tunawashukuru na kutangaza kuwa hao ni mashujaa wa Mountain View. Asante, Kampuni ya Williams kwa ukarimu wenu wa muda na rasilimali zenyu.

Hivi karibuni nilikutana na shujaa wa Mountain View anayeitwa Zeke. Mwaka uliopita Zeke alikuja katika shule yetu ili kufanya maonyesho ya tamasha ambayo yalifaidi stadi wa elimu ya muziki ili tuweze kuendelea kuwa na muziki bila malipo na masomo ya fidla kwa wanafunzi wanaotaka. Maonyesho yake ya fidla yalikuwa mazuri sana! Sijawahi kumwona mtu yeyote akicheza fidla kama yeye. Mwaka uliopita, yeye binafsi alitoa fedha za kuunga mkono masomo yetu ya muziki. Yeye ni kijana mdogo ambaye anapenda muziki na kuwasaidia wengine kujifunza muziki. Hivi karibuni aligundua fidla nyingi zisizotumiwa zilizoharibika. Zeke alichangisha pesa ili kukarabati filda hizo, na akazileta hapa Mountain View ili wanafunzi wetu wazitumie. Nimeshangazwa na kiwango chake cha ukarimu na kujali alioonyesha wanafunzi wetu na shule yetu. Zeke, wewe pia ni shujaa wetu wa Mountain View.

Ikiwa unajua shujaa mwingine wa Mountain View ambaye amefanya kitu chochote, kikubwa au kidogo, ambaye amefanya Mountain View mahali pazuri, tafadhali shiriki maelezo hayo na mimi, ili tuweze kuwasheherekea..

### Kiingilio Kilichozuiwa cha Maegesho ya Gari Kabla na Baada ya Shule

Tunapoendelea kuwatafutia njia salama zaidi kwa wanafunzi wanaowasili na kuondoka shuleni, tumegundua kwamba tukifunga kiingilio kikuu cha eneo letu la maegesho, itasababisha kusiwe na msongamano wa magari na njia salama kwa wanafunzi wetu. Ikiwa unawaleta wanafunzi au kuwachukua kwa gari, tafadhali tumia kiingilio mbele ya shule na utumie upande wa mkono wa kulia na upande wa kushoto kupita. Tafadhali epuka kuegesha gari katika maeneo mekundu ili kuwapeleka wanafunzi ndani ya shule. Pia, tafadhali kumbuka tuna maeneo ya kuwaleta/kuwachukua wanafunzi upande wa magharibi mwa shule ambayo yanasaidia kupunguza msongamano katika eneo kuu la maegesho. Ni njia nzuri mbadala.

Hakuna mfunyakazi wa wilaya au mwanafunzi anayepaswa kubaguliwa kwenye ajira au mpango au shughuli yoyote ya wilaya kwa kigezo cha umri, ulemavu, rangi, jinsi, ujinsi, taarifa za kizazi, uasilu wa taifa, ujauzito, kabila, dini, ujinsia, hadhi ya kijeshi. Wilaya imedhamiria kutoa upatikanaji uliosawa na fursa sawa katika mipango yake, huduma na ajira ikiwemo sera zake, taratibu za malalamiko, upatikanaji wa mpango, matumizi ya mali za wilaya, malazi na masuala mengine ya Fursa Sawa ya Ajira. Wialaya pia inatoa upatikanaji sawa wa mali za wilaya kwaajili ya vikundi vya vijana walioorodheshwa kwenye Sura ya 36 ya Kanuni za Marekani, ikiwemo vikundi vya skauti. Mtu ambaye ametajwa hapa chini ameteuliwa kushughulikia mahitaji na malalamishi yanayohusiana na ubaguzi usiokubalika kisheria, unyanasaji na na kulipiza kisasi: Tina Hatch, Kufuata sheria na upelelezi, 440 Mashariki 100 Kusini, Jiji la Salt Lake, Utah 84111, (801) 578-8388. Waweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Uraia, Denver, CO, (303) 844-5695.